JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA FUNDI MCHUNDO - LOCAL FUNDI

## ZABUNI NA: TR/34/2024-2025/TBS HQ /FA/01

**Dar es salaam, 06 Agosti, 2025**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia fedha za Serikali lipo katika mchakato wa ujenzi wa kituo cha kukagulia magari yanayoingia nchini kwenye ofisi zake zilizopo Ubungo. Hivyo, Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa ujenzi kuomba kazi za ufundi wa kujenga kituo hicho.

**SIFA ZA FUNDI MKUU**

1. Ajue kusoma na kuitafsiri michoro ya ujenzi.
2. Awe na uwezo wa kusimamia kazi za ujenzi.
3. Awe na ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali za ufundi.
4. Mwombaji anapaswa awe na mafundi wa fani mbalimbali na sifa zilizoainishwa.

Fundi Mkuu anapaswa kuandika barua ya maombi ya kazi hii, kwa kuzingatia masharti ya kabrasha la zabuni. Fundi anatakiwa kuonesha muda wa kumaliza kazi.

Nyaraka za zabuni hii zinapatikana Ofisi ya Manunuzi katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Ubungo.

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono kwa anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MKUU,**
**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA – TBS,**
**P.O BOX 9524,**
**UBUNGO, DAR ES SALAAM.**

Mwisho wa kupokea maombi ni **Tarehe 12/08/2025** siku ya Jumatatu saa 9:30 Jioni. na Ufunguzi utafanyika saa 10:00 Jioni katika Ofisi za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Ubungo.

**MASHARTI YA JUMLA**

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18;
2. Mwombaji aambatishe picha ndogo (passport size) mbili za rangi katika barua yake ya maombi;
3. Maombi yote yaambatane na njia za mawasiliano kama vile namba za simu, barua pepe au anuani za makazi;
4. Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya Fax, Telex na Telegraphic system na posta hayatapokelewa;
5. Cheti cha ufundi ni sifa ya ziada kwa mwombaji;
6. Barua ya mdhamini anayeishi Wilaya ya Ubungo mwenye mali zisizohamishika;
7. Kutokana na uharaka wa kazi hiyo mwombaji awe tayari kufanya kazi siku za mwisho wa wiki (weekend) na siku za mapumziko pale itakapolazimu;
8. Fundi Mkuu anatakiwa kujaza Jedwali la bei ya ufundi (Schedule of Labor) ambalo linajumuisha gharama zake pamoja na mafundi wengine wa aina mbalimbali na wasaidizi/vibarua watakaomsaidia kufanya kazi;
9. Kabla ya kujaza gharama za ufundi (Schedule of Labor) Fundi Mkuu anaruhusiwa kufika na kuangalia eneo la kazi kwa gharama zake mwenyewe;
10. Shirika lina uwezo wa kufuta mchakato huu muda wowote bila gharama yoyote;
11. Shirika halilazimiki kumchagua fundi mwenye gharama ya chini au ya juu. Uteuzi wa mafundi utazingatia miongozo, taratibu, Sheria na kanuni za Manunuzi.
12. Uteuzi wa Fundi utazingatia vigezo vilivyotajwa hapo juu pamoja na muongozo, taratibu, sheria na kanuni za manunuzi GN 446.

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka
**MENEJA UHUSIANO NA MASOKO**

**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023